JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA WA FEDHA 2021/22 KWA LUGHA RAHISI

# Toleo la Wananchi

**Imetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Policy Forum**

policy forum

## ORODHA YA VIFUPISHO

1. EFD – Mashine ya Elektroniki ya Kodi
2. EACOP – Bomba la Mafuta ghafi la Afrika Mashariki
3. GePG – Mfumo wa Malipo ya Kielektroniki ya Serikali
4. GN – Tangazo la Serikali
5. MW – Megawati
6. MSCL – Kampuni ya Huduma za Meli
7. NHIF – Mfuko wa Bima ya Afya
8. NGOs – Taasisi Zisizo za Serikali
9. REA – Wakala wa Umeme Vijijini
10. SGR – Reli ya Kiwango cha Kimataifa
11. ICT – Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
12. TANROADS – Wakala wa Barabara Tanzania
13. TARURA – Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini
14. TMA – Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
15. TBC – Shirika la Utangazaji Tanzania
16. UVIKO 19 – Ugonjwa wa Virusi vya Korona
17. VAT – Kodi ya Ongezeko la Thamani

## 1. Maana ya Bajeti ya Serikali Toleo la Wananchi

Bajeti ya Serikali Toleo la Wananchi ni Kijitabu kinachoelezea mipango na bajeti ya Serikali kwa muhtasari na lugha rahisi inayoweza kueleweka kwa Mwananchi wa kawaida na wadau mbalimbali. Kijitabu hiki kinamsaidia mwananchi kuielewa na kuifahamu bajeti ya Serikali hivyo kuhamasisha dhana ya uwazi na uwajibikaji katika kusimamia fedha za umma.

## 2. Bajeti ya Serikali

Bajeti ya Serikali ni makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha husika ambao utekelezaji wake huanza tarehe 01 Julai hadi 30 Juni. Bajeti ya Mwaka 2021/22 imeandaliwa kwa kuzingatia: Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Sheria ya Bajeti, SURA 439; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/22.

## 3. Vipaumbele vya Bajeti

Bajeti hii imelenga kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika maeneo matano (5) ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Maeneo hayo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.




## 4. Sera za Bajeti na Uchumi Jumla

### 4.1 Misingi, Malengo na Shabaha za Uchumi Jumla

Misingi, malengo na shabaha mahsusi za uchumi jumla kwa mwaka 2021/22 ni kama ifuatavyo:

i. Pato Halisi la Taifa kukua kwa asilimia 5.6 mwaka 2021;
ii. Kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ubaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya wastani wa asilimia 3.0 – 5.0;
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa;
iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa;
v. Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0; na
vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 4.2 Sera na Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato

Katika kuimarisha mapato ya ndani, Serikali itatekeleza sera zifuatazo:

i. Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuweka mazingira rafiki kwa mlipakodi;
ii. Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ikiwemo matumizi ya GePG na EFD; na
iii. Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato.

Pamoja na hatua hizo za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali itaendelea kuimarisha soko la ndani la fedha na kukopa kwa utaratibu wa udhamini kutoka taasisi za udhamini wa mikopo.


### 4.3 Sera za Matumizi


Sera za Matumizi katika mwaka 2021/22 zinajumuisha yafuatayo:

i. Kuelekeza fedha katika maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya;
ii. Kuhakikisha nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa;
iii. Kudhibiti uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni;
iv. Kuendeleza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma; na
v. Kusisitiza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali.


## 5. Mapato na Matumizi ya Serikali

Serikali imepanga kukusanya na kutumia shilingi trilioni 36.68. Mapato hayo yatakusanywa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, misaada na mikopo ya ndani na nje ya nchi. Maeneo ya matumizi ya Serikali ni pamoja na deni la Serikali, mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo.








## 6. Ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa




## 7. Mgawanyo wa Bajeti ya Serikali Kisekta

Bajeti ya Serikali imeelekezwa katika maeneo saba ya kisekta kama ilivyoainishwa kwenye **Kielelezo Na. 1.**




*Kielelezo Na. 1: Mgawanyo wa Bajeti Kisekta*

## 7.1 Elimu

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 5.26 sawa na asilimia 14 ya Bajeti. Maeneo ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi trilioni 4.04** kwa ajili ya kugharamia elimu ya awali, msingi, na sekondari, vyuo vya ualimu, ukaguzi wa shule, elimu ya watu wazima na elimu isiyo rasmi;

ii. **Shilingi bilioni 976.8** kwa ajili ya elimu ya juu sayansi na teknolojia;

iii. **Shilingi bilioni 137.6** kwa ajili ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; na

iv. **Shilingi bilioni 99.5** kwa ajili ya matumizi ya huduma za utawala.



*Vyumba Vipya vya Madarasa Shule ya Msingi King'ong'o*

## 7.2 Afya

Sekta hii imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.02 sawa na asilimia 5.5 ya Bajeti. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:


i. **Shilingi bilioni 873.7** ni kwa ajili ya kuboresha huduma na miundombinu ya afya katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya;

ii. **Shilingi bilioni 824.2** kwa ajili ya kuboresha huduma za tiba na miundombinu katika hospitali za rufaa ngazi ya kanda na taifa;


iii. **Shilingi bilioni 259.2** kwa ajili ya huduma za kinga ikiwemo ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo;

iv. **Shilingi bilioni 59.5** kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala na rasilimali watu katika utoaji wa huduma za afya; na

v. **Shilingi bilioni 2.6** kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya na miundombinu katika hospitali za rufaa za mikoa.



*Mtambo wa matibabu ya moyo*




## 7.3 Huduma za Utawala na Deni la Serikali

Serikali imetenga shilingi trilioni 14.4 sawa na asilimia 39.2 ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya matumizi katika sekta hii kama ifuatavyo:

i. **Shilingi trilioni 8.83** kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali;
ii. **Shilingi trilioni 3.03** kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala pamoja na maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika mwaka 2022;




iii. **Shilingi trilioni 2.34** kwa ajili ya shughuli za fedha na uchumi; na
iv. **Shilingi bilioni 191.9** kwa ajili ya shughuli za mambo ya nje.

## 7.4 Ulinzi, Usalama na Utii wa Sheria

Serikali imetenga shilingi trilioni 3.53 sawa na asilimia 9.6 ya Bajeti ya Serikali. Matumizi katika sekta hii ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi trilioni 2.36** kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama;
ii. **Shilingi bilioni 931.8** kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha amani, utii wa Sheria, usalama wa raia na mali zao; na
iii. **Shilingi bilioni 243.7** kwa ajili ya utawala wa Sheria kwa kusimamia mifumo ya Sheria.

## 7.5 Maendeleo ya Uchumi

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 8.33 sawa na asilimia 22.7 ya Bajeti ya Serikali zitakazotumika kugharamia sekta ndogo za: kilimo; nishati; madini; ujenzi, uchukuzi na mawasiliano; maliasili, utalii na mazingira; viwanda na biashara; pamoja na kazi, maendeleo ya vijana na kukuza ujuzi.

### 7.5.1 Kilimo

Sekta ndogo ya kilimo imetengewa shilingi bilioni 630.4. Baadhi ya matumizi ni kama ifuatavyo:


i. **Shilingi bilioni 120.9** kwa ajili ya maendeleo ya mifugo na uvuvi ikijumuisha Shilingi bilioni 50 za ujenzi wa bandari ya uvuvi;
ii. **Shilingi bilioni 63.8** kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya kilimo;
iii. **Shilingi bilioni 48.2** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa;
iv. **Shilingi bilioni 46.7** kwa ajili ya kutoa huduma za utafiti na ugani kwenye kilimo; kusimamia soko la bidhaa za kilimo; kusimamia upatikanaji wa masoko na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo;
v. **Shilingi bilioni 32.4** kwa ajili ya mradi wa udhibiti wa uchafuzi wa Sumukuvu kuepusha maradhi

yanayotokana na sumu hiyo kwenye nafaka;

vi. **Shilingi bilioni 14** kwa ajili ya kununua, kuhifadhi na kusambaza nafaka kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula nchini;

vii. **Shilingi bilioni 13.3** kwa ajili ya uzalishaji, upatikanaji na udhibiti wa ubora wa pembejeo kama vile matrekta, mbolea, na mbegu; na

viii. **Shilingi bilioni 6.5** kwa ajili ya kuendeleleza na kuimarisha Vyama vya Ushirika.



*Vihenge vya kuhifadhia nafaka Babati – Manyara*

### 7.5.2 Madini

Sekta ndogo ya madini imetengewa shilingi bilioni 66.73 kwa ajili ya maeneo ya kipaumbele yafuatayo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; na kuvutia biashara ya madini kati ya Tanzania na nchi nyingine.



*Hafla ya kukabidhi jiwe la Tanzanite lenye uzito wa kilo 6.33*

### 7.5.3 Nishati


Sekta ndogo ya Nishati imetengewa shilingi trilioni 2.36 kwa ajili ya kugharamia maeneo yafuatayo:

i. **Shilingi trilioni 1.53** kwa ajili ya miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo Bwawa la Julius Nyerere Megawati 2,115; Maporomoko ya Maji ya Rusumo Megawati 80; Ruhudji Megawati 358; na Rumakali Megawati 80;


ii. **Shilingi billioni 414.3** kwa ajili ya kugharamia awamu ya tatu ya mradi wa kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijni (REA);

iii. **Shilingi bilioni 278.3** kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme za Rufiji – Chalinze, Kinyerezi hadi Dodoma, Iringa – Singida – Shinyanga na Singida - Arusha – Namanga; na

iv. **Shilingi bilioni 18.9** kwa ajili ya kugharamia miradi ya petroli na gesi asilia ikiwemo usambazaji wa gesi asilia viwandani, utafiti wa mafuta na gesi asilia, kuchakata na kusindika gesi asilia, na uimarishaji wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja.



*Ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere*




### 7.5.4 Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Serikali imetenga shilingi trilioni 4.38 kwa ajili ya sekta ndogo ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele yaliyotengewa fedha ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 897.0** kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR);
ii. **Shilingi bilioni 722.2** zimetengwa kupitia TARURA kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za mijini na vijijini kwa ngazi za halmashauri;
iii. **Shilingi bilioni 635.9** zimelekezwa TANROADS kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara nchini;
iv. **Shilingi bilioni 450.0** kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya na matengenezo ya ndege;
v. **Shilingi bilioni 294.8** kwa ajili ya Mfuko wa Reli;
vi. **Shilingi bilioni 170.0** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano;
vii. **Shilingi bilioni 135.0** kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa meli kupitia Wakala wa Meli;
viii. **Shilingi bilioni 63.97** zitatumika katika ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya mikoa;
ix. **Shilingi bilioni 30.0** zimetengwa kwa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kwa ajili ya ununuzi wa rada na miundombinu yake; na
x. **Shilingi bilioni 15.3** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa vivuko.



*Ujenzi wa meli mpya (Mv.Mwanza Hapa Kazi Tu)*



*Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR)*
*Dar es Salaam – Morogoro*

### 7.5.5 Maliasili, Utalii na Mazingira

Serikali imedhamiria kukuza utalii na kuendeleza maliasili kwa kutenga shilingi bilioni 556.63. Fedha hizi zimelenga kuimarisha huduma za utalii ulioathirika na UVIKO 19; kutunza na kulinda maliasili na malikale; pamoja na utunzaji wa mazingira asilia. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 346.1** kwa ajili ya kuendeleza uhifadhi katika Hifadhi za Taifa na Eneo la Uhifadhi Ngorongoro;
ii. **Shilingi bilioni 152.8** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya utalii ikiwemo barabara na madaraja;
iii. **Shilingi bilioni 23.0** kwa ajili ya kugharamia uhifadhi wa misitu na nyuki;
iv. **Shilingi bilioni 15.0** kugharamia Taasisi za Utafiti na Mafunzo ya maliasili na utalii**;** na
v. **Shilingi bilioni 14.7** kwa ajili ya shughuli za vivutio vya utalii.



*Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro*

### 7.5.6 Viwanda na Biashara

Serikali imetenga shilingi bilioni 291.9 kwenye Sekta ndogo ya Viwanda na Biashara kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo:

i. **Shilingi bilioni 23.1** kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara;
ii. **Shilingi bilioni 20** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya upimaji wa magari na bidhaa nyinginezo;
iii. **Shilingi bilioni 19.7** kwa ajili ya kugharamia utafiti, ugunduzi na mafunzo ya elimu ya biashara; na
iv. **Shilingi bilioni 12.7** kwa ajili ya uendelezaji wa bidhaa za ngozi na miundombinu ya kuchakata mafuta ya kula.



*Kiwanda cha bidhaa za ngozi gereza kuu Karanga – Moshi*

### 7.5.7 Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi

Serikali imetenga shilingi bilioni 77.7 kwa ajili ya kugharamia masuala ya ukuzaji ajira na kazi ili kuhakikisha nguvu kazi ya Taifa inapata ujuzi stahiki pamoja na kuongeza fursa za ajira. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 67.7** kwa ajili ya kuwezesha Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kukuza ajira na kipato;
ii. **Shilingi bilioni 9.0** kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi Nchini; na
iii. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.



## 7.6 Hifadhi ya Jamii

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 1.85 sawa na asilimia 5.1 ya Bajeti ya Serikali. Maeneo yaliyozingatiwa ni pamoja na:

i. **Shilingi trilioni 1.57** michango ya serikali kwa ajili ya mifuko ya hifadhi ya jamii pamoja na mafao ya viongozi wastaafu;
ii. **Shilingi bilioni 242.3** kwa ajili ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF); na
iii. **Shilingi bilioni 38.34** kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za msingi kwa wazee wasiojiweza na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

## 7.7 Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 1.29 sawa na asilimia 3.5 ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali zinazohusu maji, makazi na maendeleo ya jamii.

### 7.7.1 Maji

Serikali imedhamiria kumpa unafuu mwanamke katika kufanya shughuli zake za kiuchumi, lengo likiwa ni kumtua mama ndoo kichwani. Hivyo, Serikali imetenga shilingi bilioni 706.2 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kipaumbele ikiwemo miradi ya kusambaza maji mijini na vijijini. Baadhi ya maeneo yatakayogharamiwa ni pamoja na:

i. **Shilingi bilioni 326.4** kwa ajili ya mradi wa kusambaza maji vijijini na usafi wa mazingira;
ii. **Shilingi bilioni 140.5** kwa ajili ya mradi wa kukarabati miundombinu na kusambaza maji mijini;
iii. **Shilingi bilioni 51.0** kwa ajili ya mradi wa maji safi na usafi wa mazingira katika jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani;
iv. **Shilingi bilioni 37.5** kwa ajili ya mradi wa kutambua, kutunza, kusimamia na kuendeleza rasilimali maji;
v. **Shilingi bilioni 27.4** kwa ajili ya mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Tinde hadi Shelui.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akifungulia maji kama ishara ya uzinduzi wa mradi wa Maji utakaohudumia Mji wa Misungwi na maeneo ya pembezoni*




### 7.7.2 Ardhi, Nyumba na Makazi

Sekta ndogo ya Ardhi, Nyumba na Makazi imetengewa shilingi bilioni 104.2 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kipaumbele. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni: kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani; kuboresha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa njia za kieletroniki; kuimarisha alama za mipaka ya kimataifa baina ya Tanzania na nchi inazopakana nazo; upangaji miji, upimaji na urasimishaji wa makazi.




### 7.7.3 Maendeleo ya Jamii

Sekta ndogo ya Maendeleo ya Jamii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 426.6 kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma za ustawi na maendeleo ya jamii pamoja na kuongeza ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miongoni mwa maeneo ya vipaumbele na fedha zilizotengwa ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 7.4** kwa ajili ya ukarabati wa majengo na miundombinu katika makazi ya wazee yaliyopo Chazi, Kolandoto, Magugu, Nunge, Ipuli, Fungafunga, Bukumbi, Sukamahela na Mwanzage;
ii. **Shilingi bilioni 3.6** kwa ajili ya ukarabati na ujenzi katika Taasisi za Maendeleo ya Jamii Rungemba, Uyole, Mlale na Monduli;
iii. **Shilingi bilioni 1.4** kwa ajili ya programu za kutokomeza ukatili wa kijinsia katika jamii; na
iv. **Shilingi milioni 400.0** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa mahabusu ya watoto katika mkoa wa Mtwara;
v. **Shilingi milioni 400.0** kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

## 7.8 Habari, Michezo na Utamaduni

Shilingi bilioni 54.7 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza na kukuza habari, utamaduni, Sanaa na michezo nchini. Miongoni mwa maeneo ya vipaumbele na fedha zilizotengwa ni kama ifuatavyo:

i. **Shilingi bilioni 10.5** kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa viwanja vya burudani na michezo;
ii. **Shilingi bilioni 5.0** kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC);
iii. **Shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Vyuo vya Utamaduni na Sanaa;
iv. **Shilingi bilioni 1.3** kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Michezo Mallya;
v. **Shilingi bilioni 1.0** kwa ajili ya kuboresha utoaji wa habari kwa umma; na
vi. **Shilingi milioni 515.0** kwa ajili ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

## Maboresho ya Mifumo ya Kodi, Ada na Tozo

Serikali imefanya maboresho ya mifumo ya kodi, ada na tozo kwa lengo la kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika sekta ya kilimo na viwanda, na kuongeza mapato ya Serikali. Baadhi ya maeneno yaliyoboreshwa ni kama ifuatavyo:

1. **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148**
   a. Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye;
      i. Madini na makinikia yatakayoingizwa nchini kwa ajili ya kuchenjuliwa, kuongezewa thamani na kuuzwa kwenye masoko ya madini yanayotambulika nchini;
      ii. Huduma za bima ya mifugo;
      iii. Bidhaa na huduma zitakazoingizwa au kununuliwa hapa nchini kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mafuta ghafi (EACOP); na
      iv. Bidhaa na huduma zitakazotumika kwenye miradi inayotekelezwa na Taasisi zisizo za kiserikali (NGOs); na
   b. Kurudisha utaratibu wa kurejesha Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara na kutumika Tanzania Zanzibar.

2. **Sheria ya Kodi ya Mapato SURA 332**
   i. Kutoza asilimia 8 kwa kiwango cha chini ya Kodi ya Mapato yanayohusiana na ajira;
   ii. Kusamehe Kodi ya Mapato kwenye hatifungani za Serikali;
   iii. Kurejesha utaratibu wa Mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutoa msamaha kupitia tangazo la Serikali (GN) bila sharti la kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za wafadhili; na
   iv. Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia mbili (2) kwenye malipo yanayohusisha mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yanapouzwa kwenye kampuni na mashirika yote yanayojihusisha na usindikaji na ununuzi wa mazao.

3. **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**
   i. Kupunguza Ushuru wa Bidhaa kwenye bia zinazotengenezwa kwa kutumia shayiri iliyozalishwa hapa nchini kutozwa shilingi 620 kwa lita;
   ii. Kuanzisha tozo ya asilimia 10 kwenye nyuzi na kamba za plastiki (synthetic fibres) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi au kuzalishwa hapa nchini isipokuwa zile zinazotumika kwenye uvuvi; na
   iii. Kuanzisha tozo ya ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye pikipiki zilizotumika kwa zaidi ya miaka 3 zinazoingizwa nchini.

4. **Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**
   i. Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mwendokasi;
   ii. Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarn);
   iii. Kutoza asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye makopo ya kuhifahdia maziwa (milk cans); na
   iv. Kutoza asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mbolea kwa utaratibu wa *duty remission*.

5. **Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, SURA 178**
   Kufuta tozo ya asilimia 6 iliyokuwa ikitozwa kwa ajili ya kulinda thamani ya mkopo wa elimu ya juu kwa wanufaika.

6. **Sheria ya Kodi ya Majengo, SURA 289**
   Kutoza kodi ya majengo ya kiwango cha shilingi 1000 kwa mwezi kwenye nyumba za kawaida zenye mita moja ya umeme ambayo itakatwa kwenye ununuzi wa umeme (LUKU) na kutoza kodi ya majengo ya kiwango cha shilingi 5000 kwa mwezi kwa kila ghorofa au *apartment* zenye mita moja ya umeme ambayo itakatwa kwenye ununuzi wa umeme (LUKU).

7. **Sheria ya Ardhi, SURA 113**
   i. Kupunguza kiwango cha tozo ya kodi ya ardhi kutoka asilimia 2.5 hadi asilimia 0.5 kwa umiliki mpya wa ardhi na
   ii. Kupunguza kiwango cha tozo ya kodi ya ardhi kutoka asilimia 1.0 hadi asilimia 0.5 Kutoza asilimia 0.5 kwa urasimishaji.

8. **Sheria ya Usajili wa Magari SURA 124**
   Kupunguza kiwango ya malipo ya usajili wa magari kwa namba binafsi kutoka kwa shillingi 10,0000,000 hadi shilingi 5,000,000 kila baada ya miaka mitatu.

9. **Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168**
   Kupunguza kiwango cha adhabu ya makosa ya barabarani kwa bajaji na pikipiki kutoka shilingi 30,000 hadi 10,000 kwa kila kosa.

## Hatua Nyingine za Mapato

Serikali itatumia njia nyingine za kuongeza mapato ili kufanikisha utekelezaji wa ujenzi wa barabara za mijini na vijijini; upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini; afya na bima ya afya kwa wote; elimu na miradi ya kielelezo ya Bwawa la Kufua umeme wa maji la Mwalimu Nyerere na Reli ya Kisasa (SGR). Hatua hizo ni pamoja na kufanya marekebisho kwenye sharia zifuatazo:

1. **Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220**
   Kuongeza ushuru wa barabara kwa shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli.

2. **Sheria ya Petroli, SURA 392**
   Kuongeza tozo ya mafuta taa kutoka shilingi 150 hadi shilingi 250 kwa lita.

3. **Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306**
   i. Kutoza tozo ya shilingi 10 hadi shilingi 10,000 katika kila muamala wa kutuma au kutoa pesa; na
   ii. Kutoza kiasi cha shilingi 10 hadi shilingi 200 kwa siku kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji.

Jedwali 1: Muhtasari wa Mgawanyo wa Bajeti Kisekta

| Sekta | | Bajeti 2021/22 (bilioni) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| **Elimu** | | **5,257.29** | **14.33** |
| **Afya** | | **2,019.19** | **5.50** |
| **Huduma za Utawala na Deni la Serikali** | | **14,396.87** | **39.25** |
| | Huduma za Utawala (bila Deni la Serikali) | 5,562.05 | 15.16 |
| | Deni la Serikali | 8,834.82 | 24.08 |
| **Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama** | | **3,532.72** | **9.63** |
| **Maendeleo ya Uchumi** | | **8,330.67** | **22.71** |
| | Kilimo | 630.36 | 1.72 |
| | Madini | 66.73 | 0.18 |
| | Nishati | 2,385.95 | 6.50 |
| | Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | 4,377.54 | 11.93 |
| | Maliasili, Utalii na Mazingira | 556.63 | 1.52 |
| | Viwanda na Biashara | 291.88 | 0.80 |
| | Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi | 21.59 | 0.06 |
| **Hifadhi ya Jamii** | | **1,853.41** | **5.05** |
| **Maji, Nyumba na Maendeleo ya Jamii** | | **1,291.75** | **3.52** |
| | Maji | 706.21 | 1.93 |
| | Ardhi, Nyumba na Makazi | 104.20 | 0.28 |
| | Maendeleo ya Jamii | 426.60 | 1.16 |
| | Habari, Michezo na Utamaduni | 54.74 | 0.15 |
| **Jumla** | | **36,681.90** | **100.00** |

**NYARAKA REJEA ZA BAJETI**

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka rejea za Serikali zilizotumika kuandaa Kijitabu cha Bajeti Toleo la Mwananchi kwa mwaka 2021/22:

1. Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025;
2. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22– 2025/26;
3. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2020;
4. Randama za Mipango ya Muda wa Kati na Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati ya mwaka 2021/22;
5. Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/22;
6. Hotuba za Bajeti za Wizara za Mwaka wa Fedha 2021/22;
7. Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2021/22;
8. Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021;
9. Sheria ya Matumizi ya Mwaka 2021;
10. Sheria ya Bajeti 2015, SURA 439; na
11. Vitabu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 (Juzuu Na. I, II, III na IV).

Ili kupata baadhi ya nyaraka hizi na matoleo yaliyotangulia ya Vitabu vya Bajeti ya Serikali Toleo la Mwanachi, unaweza kutembelea tovuti ya:

- Wizara ya Fedha na Mipango (www.mof.go.tz)
- Policy Forum (www.policyforum.or.tz)

## Kwa maelezo zaidi kuhusu Bajeti ya Serikali

Unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mchakato wa uandaaji wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo: Nyaraka zenye taarifa za Bajeti ya Serikali (***angalia orodha ya nyaraka za rejea***) hususan, nakala ngumu ya Vitabu vya Bajeti ya Serikali ambavyo vinapatikana Wizara ya Fedha na Mipango S.L.P 2802, Dodoma.

Kumbuka kwamba ni haki yako kujua bajeti hii na taarifa nyingine zinazohusiana na Bajeti ya Serikali. Ongea na Viongozi wako kuhusu taarifa hizi na washirikishe watu wengine katika jamii unayoishi nayo.

**Kwa maoni yako jaza ukurasa huu na kutuma Wizara ya Fedha na Mipango**

Toa maoni yako kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/22
-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
----------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, unahitaji ufafanuzi zaidi ya uliotolewa katika kijitabu hiki? □NDIYO
□HAPANA
Kama jibu ni NDIYO Je, unahitaji ufafanuzi katika eneo gani?

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------
--------------------------------------------------------------------------------------------------------------

Je, ni kwa kiasi gani kijitabu hiki kimekusaidia?
□ Kiasi kikubwa □ Wastani □ Hakikunisaidia

Je, ni kwa kiasi gani kijitabu hiki kilikuwa rahisi kusoma na kueleweka?
□ Rahisi □ Wastani □ Ngumu

Je, umepataje kijitabu hiki (weka alama ya **V** kwenye kisanduku ulichochagua)?

- Tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango □
- Tovuti ya Jukwaa la Sera □
- Taasisi za Serikali □
- Nyingine □ (Tafadhali taja)

Tuma maoni yako katika anuani ifuatayo

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Fedha na Mipango,**
**Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali,**
**Mtaa wa Hazina,**
**Mji wa Serikali – Mtumba,**
**40468 Dodoma,**
**Sanduku la Barua 2802,**
**DODOMA-TANZANIA**

Au tuma kwa njia ya barua pepe kwa:
**ps@mof.go.tz**